# Kuelekea Kura ya Maoni

## Maoni ya Watanzania kuhusu Katiba Inayopendekezwa








## 1. Utangulizi

Katiba huakisi maafikiano kati ya wananchi na dola, na Katiba hiyo huainisha haki na wajibu wa pande zote na kuweka mfumo wa utawala wa nchi. Mchakato wa mabadiliko ya Katiba hapa Tanzania ulianza rasmi mwaka 2013 na ulitakiwa kufikia kikomo kwa kura ya maoni iliyopangwa kufanyika mwezi Aprili 2015.

Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa ni matokeo ya safari ndefu. Tarehe 3 Juni 2013, baada ya mchakato mpana wa kukusanya maoni ya wananchi kwa njia ya mikutano, mahojiano na maoni yaliyotolewa kwa maandishi, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilikabidhi rasimu ya kwanza ya Katiba. Rasimu hiyo ilianzisha majadiliano makubwa na wananchi walitoa maoni yao kuhusu mapendekezo yaliyomo kwa njia rasmi na zisizo rasmi. Maoni ya wananchi yakawa msingi wa kufanya marekebisho mbalimbali. Rasimu ya pili iliandaliwa na kukabidhiwa rasmi tarehe 30 Desemba 2013. Rasimu ya pili ikafikishwa mbele ya Bunge la Katiba. Wabunge wa kuchaguliwa waliungana na wajumbe walioteuliwa kutoka Asasi za Kiraia pamoja na jamii mbalimbali Dodoma na kuijadili rasimu ya pili ya katiba.

Bunge Maalumu la Katiba lilitawaliwa na mifarakano mingi. Hatimaye wajumbe kutoka vyama vya upinzani wakajitoa. Hata hivyo, baadhi ya wajumbe waliendelea kuhudhuria vikao vya Bunge Maalumu la Katiba, na kutoa mapendekezo ya marekebisho na hatimaye kuwasilisha Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa tarehe 8 Oktoba 2014.

Mchakato mzima uliozaa Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa umeghubikwa na mabishano mengi. Kwa upande mmoja, baadhi ya wananchi wameonyesha kuridhishwa na jinsi Katiba Inayopendekezwa inavyotetea wananchi ambao hapo nyuma hawakutambulika kimamilifu, kwa mfano wanawake na watu wenye ulemavu. Kwa upande mwingine suala

Muhtasari huu umeandikwa na Youdi Schipper, Angela Ambroz, na Elvis Mushi
Na umeandaliwa na Twaweza East Africa
Umetolewa Machi 2015

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | uwazi@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti

la “Muungano” – na uhusiano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar – limebaki kuwa jambo linalohitaji muafaka unaoridhisha pande zote. Pamoja na hilo, mambo yanayohusu kuimarisha uwazi, uwajibikaji wa watumishi wa umma na kupunguza madaraka ya Rais, ni mambo yaliyopewa umuhimu wakati wa kukusanya maoni ya wananchi. Bunge Maalum la Katiba likawa na mtazamo mbadala. Baadhi ya wachambuzi wanalalamika kwamba Katiba Inayopendekezwa inawiana na matakwa ya chama tawala tu. Wanaoiunga mkono Katiba Inayopendekezwa wanaona kuwa rasimu hiyo inawakilisha mawazo ya wananchi.

Hiki ni kipindi cha wananchi kufanya maamuzi  mazito. Twaweza imetumia *Sauti za Wananchi* kukusanya maoni yao kuhusu mchakato wa mabadiliko ya Katiba, na Katiba Inayopendekezwa yenyewe. Mwananchi wa kawaida anaichukuliaje Katiba Inayopendekezwa? Je wanaunga mkono jitihada za wapinzani kuvisusia vikao vya Bunge Maalum ya Katiba? Je wana maoni gani kuhusu kubadilishwa kwa baadhi ya vipengele vya rasimu ya pili ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba? Je wananchi wataikubali au kuikataa rasimu ya Katiba Inayopendekezwa?

Ripoti hii ni muhtasari wa maoni ya wananchi wa Tanzania Bara juu ya Katiba Inayopendekezwa. Takwimu hizi zinatokana na duru ya 29 ya *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza Afrika kwa njia ya simu za mkononi wenye uwakilishi wa kitaifa (www.twaweza.org/sauti). Jumla ya wahojiwa 1,399 walipigiwa simu kati ya Januari 27 na Februari 17, 2015. Matokeo mengine yanatokana na duru ya tano ya *Sauti za Wananchi*, (iliyowahoji watu 1,708 kati ya Julai 16 na Julai 30, 2013) na duru ya 14 ya *Sauti za Wananchi* (iliyowahoji watu 1,550 kati ya Februari 12 na Machi 4, 2014).

Matokeo muhimu kwenye muhtasari huu:
- Wananchi wamejigawa kati ya Katiba Inayopendekezwa (asilimia 39 wanaiunga mkono) na rasimu ya pili ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba (asilimia 41 wanaiunga mkono),
- Wananchi wanaunga mkono vifungu vinavyoongeza uwajibikaji,
- Watu saba kati ya kumi (asilimia 68) wanapinga kitendo cha Ukawa kususia vikao vya Bunge la Katiba
- Wananchi watatu kati ya wanne (asilimia 75) hawana mpango wa kuitikia wito wa Ukawa wa kutoshiriki Kura ya Maoni
- Mtu mmoja kati ya wawili Tanzania Bara (asilimia 52) ana mpango wa kuiunga mkono Katiba Inayopendekezwa atakapopiga Kura ya Maoni.


# 2. Maoni ya wananchi kuhusu Katiba Inayopendekezwa

## Jambo la 1: Wananchi watatu kati ya wanne wanaielewa Katiba Inayopendekezwa

Wananchi watatu kati ya wanne wanafahamu kuwa Bunge la Katiba limepitisha Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa mwezi Oktoba 2014. Lakini asilimia 72 ya wananchi hawafahamu ni

wapi wanaweza kupata nakala ya Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa. Aidha, asilimia 60 ya wananchi hawazifahamu hatua zitakazochukuliwa kumaliza mchakato wa kubadili Katiba.

**Kielelezo 1: Je unafahamu kuhusu Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa na Bunge Maalumu la Katiba pamoja na mahali unapoweza kupata nakala yake?**





**Chanzo:** *Sauti za Wananchi* - Duru ya 29 (Januari--Februari 2015)

## Jambo la 2: Wananchi wamejigawa kati ya Katiba Inayopendekezwa na rasimu ya pili ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba

Twaweza ilikusanya maoni ya wananchi kuhusu tofauti zilizopo kati ya rasimu ya pili na rasimu ya Katiba Inayopendekezwa. Wachache (asilimia 20) hawana maoni kuhusu tofauti zilizopo kati ya rasimu hizo mbili. Wenye maoni wamejigawa katikati: asilimia 39 wanapendelea rasimu ya tatu na wengi kidogo, asilimia 41 wanapendelea rasimu ya pili (kielelezo 2).

**Kielelezo cha 2: Kama ungepewa nafasi ya kuchagua, ni rasimu ipi ungeichagua kuwa Katiba ya Muungano?**





**Chanzo:** *Sauti za Wananchi* - Duru ya 29 (Januari--Februari 2015)

## Jambo la 3: Wananchi wanayo mitazamo tofauti kuhusu mabadiliko yaliyomo kwenye Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa

Asilimia 80 ya wananchi wanakubaliana na vifungu vya kuwawajibisha wabunge wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao. Vifungu hivi vilifutwa, na havipo ndani ya Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa. Hata hivyo, wananchi wengi kiasi (asilimia 60) wanaunga mkono kufutwa kwa kifungu cha kuwepo kwa serikali tatu, na kuendelea na serikali mbili (Kielelezo cha 3).

**Kielelezo cha 3: Ni kwa kiasi gani unakubaliana na uamuzi wa Bunge la Katiba kuhusu:**




**Chanzo:** *Sauti za Wananchi* - Duru ya 29 (Januari--Februari 2015)
*Inaweza kutofika asilimia 100, kwani majibu "Sifahamu" na "Sina maoni" hayakuonyeshwa.*
*Takwimu kamili zinapatikana hapa: www.twaweza.org.*

Tulipolinganisha matokeo ya duru mbili (Julai 2013 na February 2015), tuliyaona yafuatayo:

- Julai 2013, asilimia 91 ya wananchi waliunga mkono kifungu cha wabunge kuwajibishwa wanaposhindwa kutimiza wajibu wao. Idadi hiyo imepungua na kufika asilimia 80 ya wananchi katika duru hii;
- Asilimia 70 ya wananchi bado wanaunga mkono ukomo wa vipindi vya ubunge (miaka 15) kama ilivyokuwa Julai 2013;
- Kati ya asilimia 67 na 95 ya wananchi wanaendelea kuvikubali vifungu mbalimbali vinavyosisitiza uwazi;
- Asilimia 22 ya wananchi walikubaliana na mfumo wa serikali tatu hapo Julai 2013. Mfumo huo wa serikali tatu sasa unaungwa mkono na asilimia 36 ya wananchi.


## Jambo la 4: Wananchi saba kati ya kumi hawakubaliani na uamuzi wa Ukawa kususia vikao vya Bunge la Katiba.

Wananchi walio wengi (asilimia 68) wanafahamu kuhusu muungano wa vyama vya upinzani, Ukawa, na kususia kwao vikao vya Bunge la Katiba mapema mwaka 2014. Hata hivyo, idadi hiyo hiyo (asilimia 68), hawakubaliani na kitendo hicho.

Hivi karibuni, Ukawa umekuwa ukiwashawishi wananchi kususia Kura ya Maoni (iliyopangwa mwezi Aprili 2015). Kwa mara nyingine, asilimia 65 ya wananchi wanaipinga

hoja hii. Kwa uzito zaidi, wananchi watatu kati ya wanne (asilimia 75) wamejibu kuwa hawatashiriki katika kususia Kura ya Maoni (takwimu hazijaonyeshwa).

**Kielelezo cha 4: Je, ni kwa kiasi gani unakubaliana na uamuzi uliofanywa na Ukawa kujitoa kwenye Kura ya Maoni ya mwezi Aprili?**





**Chanzo:** *Sauti za Wananchi* - Duru ya 29 (Januari--Februari 2015)

## Jambo la 5: Wananchi sita kati ya kumi watajiamulia jinsi ya kupiga Kura ya Maoni.

Walipoulizwa kuhusu vyanzo vyao vya taarifa kuhusu mchakato wa kubadilisha Katiba, redio ndio chanzo kikubwa kwa wananchi walio wengi, (zaidi ya wananchi sita kati ya kumi walitaja redio kama chanzo kikuu) (Kielezo cha 5). Mtawanyiko wa vyanzo vya habari umeorodheshwa (Kielelezo cha 5).


**Kielelezo cha 5: Je, unapata wapi taarifa kuhusu mchakato wa mabadiliko ya Katiba ?**




**Chanzo:** *Sauti za Wananchi* - Duru ya 29 (Januari--Februari 2015)
*Takwimu kamili zinapatikana hapa: www.twaweza.org.*

Walipoulizwa ni nani anayeweza kushawishi uamuzi wao siku ya kupiga kura, wananchi walijibu kuwa watakuwa huru kufanya maamuzi. Wananchi sita kati ya kumi (asilimia 58) waliripoti kuwa watajiamulia wenyewe wakati wa kupiga Kura ya Maoni. Watakaofuata maoni ya serikali ni asilimia 9, CCM (asilimia 9), Ukawa (asilimia 7), marafiki (asilimia 4) na familia (asilimia 3). (Kielelezo cha 6).

**Kielelezo cha 6: Je, ni kikundi au watu gani watakaokuwa na ushawishi katika uamuzi wako wa kuipitisha au kuikataa Katiba Inayopendekezwa?**





**Chanzo:** *Sauti za Wananchi* - Duru ya 29 (Januari--Februari 2015)
*Takwimu kamili zinapatikana hapa: www.twaweza.org.*

## Jambo la 6: Nusu ya wananchi wanaamini kuwa uchaguzi mkuu ujao utaendeshwa chini ya Katiba mpya

Mmoja kati ya wananchi wawili (asilimia 47) anaamini kuwa Uchaguzi Mkuu uliopangwa kufanyika mwishoni mwa 2015, utafanyika chini ya Katiba mpya. Hata hivyo, wananchi watatu kati ya kumi (asilimia 30) wanaamini kuwa Katiba ya sasa itabaki na kutumika na mwananchi mmoja kati ya watano (asilimia 22) hana uhakika na kitakachotokea. (Kielelezo cha 7).

**Kielelezo cha 7: Je unafikiri Uchaguzi Mkuu ujao utafanyika chini ya Katiba ya sasa au Katiba mpya?**





**Chanzo:** *Sauti za Wananchi* - Duru ya 29 (Januari--Februari 2015)

## Jambo la 7: Mwananchi mmoja kati ya wawili anatarajia kuiunga mkono Katiba Inayopendekezwa

Kuungwa mkono kwa Katiba Inayopendekezwa kumekuwa kunabadilika siku hadi siku. Mwaka 2013, asilimia 45 ya wananchi walipanga kuunga mkono Katiba Inayopendekezwa siku ya Kura ya Maoni (Kielelezo cha 8). Ilipofika 2014, idadi hiyo iliongezeka kufikia asilimia 65. Mwaka 2015, idadi hiyo imepungua na kufikia asilimia 52. Wakati huo huo, idadi ya wahojiwa waliopanga kupinga Katiba Inayopendekezwa imeongezeka kidogo kutoka asilimia 21 mwaka 2014 hadi asilimia 26 mwaka 2015 (Kielelezo cha 8).

**Kielelezo cha 8: Kama Kura ya Maoni kuhusu Katiba ingefanyika leo, je ungepiga kura kupinga au kuunga mkono Rasimu ya Katiba Inayopendekezwa iliyokabidhiwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Bunge la Katiba ?**




**Chanzo:** *Sauti za Wananchi* - Duru ya 29 (Januari--Februari 2015)

# 3. Hitimisho

Swali muhimu kwa wananchi wote ni je, Katiba Inayopendekezwa itapitishwa au la wakati wa Kura ya Maoni? Kwa chama tawala, jibu la wananchi litakuwa ishara ya ushawishi wake wa kisiasa ikikumbukwa kwamba huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu. Kwa wapinzani, huu ni wakati wa kujua ni kwa kiasi gani wananchi wanawaunga mkono.

Mambo haya machache yanastahili kukumbukwa:

- Takwimu kutoka Zanzibar hazikutumiwa katika muhtasari huu. Hata hivyo, takwimu nyingine zinaonyesha kwamba asilimia 80 ya Wazanzibari wanaunga mkono mfumo wa Muungano wa Serikali Tatu na asilimia 5 hawakutaka mabadiliko yoyote katika mfumo uliopo.[1]

[1] Sauti za Wananchi, Muhtasari Na. 11, Je wananchi wanafikiri nini juu ya Katiba ? Aprili 2014.

- Wakati wote wa mchakato huu wa mabadiliko ya Katiba, wananchi wamesisitiza masuala ya uwazi na uwajibikaji mpana zaidi wa serikali na wabunge, lakini vifungu hivi vimefutwa katika rasimu ya Katiba Inayopendekezwa.
- Wakati huo huo, asilimia 52 ya wananchi wa Tanzania Bara wameripoti kuwa wataunga mkono Katiba Inayopendekezwa.

Ni muhimu kutambua pia kwamba licha ya minong'ono mingi ya kutoridhika, na mawazo yaliyotapakaa kuwa mchakato wa kuibadilisha Katiba umetekwa nyara, wananchi hawako tayari kuchukua hatua kali ya kususia Kura ya Maoni. Ukawa na washirika wao hawana budi ya kuzingatia kutoungwa mkono na wananchi katika mambo haya mawili: kususia vikao vya Bunge Maalumu la Katiba na kutaka wananchi wasishiriki katika Kura ya Maoni.

Hali ya sintofahamu ya kukubalika kwa Katiba Inayopendekezwa, inaongezeka kwa sababu ya kuwepo kwa mashaka kama Kura ya Maoni itapigwa kama ilivyopangwa mwezi Aprili 2015. Katika hotuba yake kwa Taifa ya mwishoni mwa mwezi Februari 2015, Rais aliiagiza Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba fedha za kutosha zinatolewa kwa ajili ya kuboresha daftari la wapiga kura.. Hii inaonyesha nia thabiti ya serikali kuhakikisha kuwa Kura ya Maoni inafanyika kama ilivyopangwa.

Kutokana na mashaka haya na athari za muda mrefu zitakazotokana na maamuzi yatakayofanyika katika kipindi hiki, uongozi wa makini katika ngazi zote za jamii ya Tanzania unahitajika. Serikali lazima ihakikishe kuwa mchakato wa uandikishaji na uboreshaji wa daftari la wapiga kura unafanywa kwa uadilifu na weledi, ili kuweka mazingira ya kuonyesha kuwa Kura ya Maoni itakuwa huru na ya haki, na itawakilisha maoni ya wapiga kura. Viongozi wa kisiasa na kijamii wanatakiwa kuwaongoza na kuwashawishi wananchi kwa nguvu, lakini bila kuwanyima uhuru wa maoni. Mwishowe, wakati huu, Watanzania wana wajibu wa kufanya maamuzi mazito. Ni muhimu kuyafanya maamuzi hayo kwa utashi wao, kwani kushiriki kwao kikamilifu ni dhamana kubwa.